MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Kiunzi cha Kweli-Bunilizi katika Hadithi ya “Mwendawazimu”: Mtazamo wa Uhakiki-Maeneo

Julius Shitemi*, Tom Olali, Evans Mbuthia, Alex Wanjala

*Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya*

**IKISIRI**

Kazi za Fasihi hujikita katika kueleza hadithi za kibunilizi. Hata hivyo, katika ubunifu huu kuna uwezekano mkubwa wa kupata data za kweli kuhusu maeneo, wahusika ama maudhui. Makala hii inaangazia matumizi ya nadharia ya uhakiki maeneo katika kudadavua ukweli katika bunilizi za Kiswahili. Utafiti uliteua hadithi ya “Mwendazimu” iliyoandikwa na Shake, (2000). Ulitumia mihimili ya uhakiki-maeneo: ukiukaji mipaka, mwanda wa kijamii, mwingiliano matini na mikakati ya kiuhakiki-matini: mtazamo kwingi, mpangilio-safu na fahiwa ainati. Makala inaonyesha ufanifu mkubwa wa uhakiki-maeneo kama nyenzo ya kudadavulia ukweli katika bunilizi za Kiswahili. Mapendekezo ya utafiti huu ni kuwa mtazamo wa uhakiki-maeneo utumiwe kuchambulia hadithi nyingi ili kufaidi maarifa kutokana nao.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Uhakiki-maeneo,
Ukweli,
Bunilizi

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 10 Januari 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 25 Januari 2025
Tarehe ya Kukubalika: 10 February 2025
Mtandaoni: March 2025

## 1. Utangulizi

Kazi za kisanaa ikiwemo fasihi huvyazwa kupitia ubunilizi. Roberts & Jacob (1995), wameeleza kuwa, ubunilizi ni kitu kilichoundwa au kuumbwa na mwanadamu. Binadamu daima amekuwa akibuni hadithi ainati. Hadithi hizi ziko kwenye riwaya, novela au hadithi fupi. Huenda baadhi ya wasomaji wa kazi hizi za kifasihi wasizichukulie kwa makini kwa sababu ni zao la ubunifu wa mtungaji. Hata hivyo, makala hii iliazimia kubainisha kuwa, katika ubunilizi kuna elementi nyingi za ukweli ambao umesheni katika matini za fasihi. Usomaji wa kazi hizi unaweza kutajirisha tajiriba za msomaji. Makala hii, inatumia nadharia ya uhakiki-maeneo kudhirihisha uhalisia huu.

Mbuthia (2005) ana maoni kuwa, baadhi ya hadithi fupi za Kiswahili husawiri mazingira (maeneo) kwa mapana na marefu. Ilhali, nyingine hazitilii maanani mazingira. Waandishi wanajikita katika kushughulikia maudhui. Hadithi fupi ya “Mwendawazimu” ya Shake, (2000) ina ukwasi wa matumizi ya maeneo ya kijiografia kihomotopiki. Matukio yamesimikwa katika maeneo ambamo msomaji mmaizi wa maeneo tajwa kama Tala, Kangundo, hospitali ya Mathare, kituo cha magari cha Tea Room na barabara ya Moi jijini Nairobi ataweza kunasibisha maeneo haya husika na mianda inayoibuliwa na kuvyazake kwayo. Hivyo, hadithi yenyewe inaafiki sana kuhakikiwa kiuhakiki-maeneo ili kuhusisha matukio na maeneo ambayo yanashajiisha na kushawishi utukiaji wake.

Uhakiki-maeneo ni zoezi la kiuhakiki ambalo linachunguza data za kijiografia na kuchanganulia hadithi. Uhakiki-maeneo una azma ya kuhusisha maeneo ya kijiografia yalivyosawiriwa katika hadithi za kibunilizi katika ulimwengu halisi ili kuwa kiunzi cha kuauni ufasiri wa hadithi zenyewe. Kupitia usawiri wa kihomotopiki, kiheterotopiki na kitranto. Kwa mujibu wa Tally (2011a) na Prieto (2011), usawiri wa maeneo kihomotopiki unahusu usawiri wa maeneo ya kijiografia katika hadithi kama wasomaji wanavyoyafahamu katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, hadithi ya Shake, (2000) “Mwendawazimu” inaafiki usawiri wa jiji la Nairobi. Aidha, hadithi ya Mbatiah (1996) ya “Jahanamu” ni usawiri wa eneo la makaazi ya mabanda ya Mathare, jijini Nairobi. Usawiri wa maeneo katika hadithi ya “Mwendawazimu” unaifanya kuwa faafu kuhakikiwa kupitia uhakiki-maeneo kuliko mkabala mwengine wa kuhakiki maeneo katika hadithi.

Aidha, makala hii inalenga kupanua mawazo ya makala ya Sharobeem (2015) kuhusu mgong’ano wa kitamaduni na mahusiano ya kijinsia katika hadithi tatu kutoka diwani ya “*The Thing Around your Neck*” kwa kutumia nadharia ya uhakiki-maeneo na mwanda. Makala hii inasisitiza kwamba si lazima utafiti katika hadithi fupi uhusishe hadithi nyingi ili kuvyaza data toshelevu kuchanganulia matatizo ainati ya utafiti katika fasihi. Hivyo, hadithi ya “Mwendawazimu” imejitosheleza na kujisimamia na kuhitimu kuvyaza data za kuchanganua swala la ukweli-bunilizi katika hadithi fupi za Kiswahili

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254720929733; Barua Pepe: Mulamamulamasj@students.uonbi.ac.ke

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Julius S., Tom O., Evans M., & Alex W. (2025). Kiunzi cha Kweli-Bunilizi katika Hadithi ya “Mwendawazimu”: Mtazamo wa Uhakiki-Maeneo. Jarida la Kiswahili Sanifu 2(2025), 8 – 13.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

pasi kujiegemeza katika hadithi nyingine kutoka diwani ya *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*.

### 1.1. Muhtasari wa Hadithi ya "Mwendazimu"

Hadithi ya "Mwendawazimu" imeandikwa na Shake, (2000). Inapatikana katika diwani ya *Mwendazimu na Hadithi Nyingine*. Hadithi inahusu mzee Katona ambaye alikuwa amestahafu kwa mpango wa miaka 1990 almaarufu "Golden Handshake". Alipopata habari kuwa pesa zake zilikuwa zimefika, alipanga safari kutoka kwake Kangundo hadi Nairobi. Mkewe Ndunge alimsihi aandamane naye Nairobi. Ndunge alihofia kuwa fedha za mumewe zingeibwa na majambazi. Mzee Katona alikataa. Alidai kuwa, alikuwa ameishi Nairobi miaka mingi. Angetambua jambazi akimwona mmoja.

Baada ya kutoka benki alifika katika duka la kuuza nyama lililojulikana kama New Matigari Butchery, alitarajia kupata chamcha cha Ugali kwa nyama choma. Huku akingoja matatu yake ipendayo *Kavaluku Ka City*. Alipokuwa akila agizo lake, macho yake yalikutana ana kwa ana na mwanamke mmoja mjamzito na "mumewe". Alikumbuka kumwona katika benki. Alipoona ana "mumewe" hakuendelea kufikiria kuhusu mwanamke huyo tena. Alimaliza chakula chake.

Mzee Katona alipofika kituo cha matatu, alipata matatu yake imekwisha kufika. Mlikuwa mmesalia viti vinne. Kondakta walimpokea na kumpa kiti kilichokuwa nyuma katika matatu hiyo.

Mzee Katona akiwa katika hali ya kungoja matatu ijae, yule mwanamke na "mumewe" walifika kituoni. Wawili hao wakawa wanazungumza na kondakta kwa sauti ya chini. Japo alisikia neno moja moja kama ni "mgonjwa sana". Kisha akatokea bwana mmoja ambaye alivalia magwanda ya ukasisi. Yule mwanamke mjamzito akampongeza kwa kufika. Kabla gari liondoke, kondakta alimweleza dereva jambo ambalo lilionekana kumshangaza. Hata hivyo, dereva alipiga gari moto. Kutanabahi, abiria walishangaa kuwa gari liliacha njia ya kuelekea Kangundo. Abiria walijuzwa kuwa garini mna mgonjwa ambaye huenda atazusha zahama akiambiwa ashuke. Hivyo, walikuwa wanampeleka hospitali ya wangonjwa ya Mathare. Mzee Katona aliangaza macho kuona nani alikuwa akitajwa. Macho yake yalitwaa kwa mzee mmoja aliyekuwa akizinzia, Mzee Katona akamshuku kuwa ndiye mgonjwa.

Matatu ilipofika karibu na hosipitali ya Mathare, "Kasisi" akaomba gari lisimamishwe kuwa haikuwa na haja ya kuingia ndani. Akisema hayo, mama mjamzito alikuwa amemkabili Mzee Katona akimsihi washuke. Alimwita babake. Huku kasisi akitambulisha kama mjomba Luka. Mzee Kantona alijaribu kukanusha kuwa hakujua hao "jamaa zake". Kwa msaada wa abiria wengine, Mzee Katona alishukishwa kwa nguvu.

Walipofikia nje, gari liliondoka. Kasisi alimshika Mzee Kantona shingoni na kumpiga goti tumboni. Huku, yule mjamzito alisikika akishukuru Mungu kwa kuwapa tijara. Wapita njia hawakutuhumu chochote. Kwa maana, walikuwa wamezoea kuona wendazimu ambao walikataa kuingizwa hospitalini. Hivyo, ndivyo Mzee Katona alivyopoteza elfu mia mbili za kiinua mgomgo chake.

## 2. Mapitio ya Maandishi

Swala la ukweli katika kazi za kibunilizi limeshughulikiwa na wahakiki wengi. Blocker (1970) anaeleza kuwa katika fasihi, ili kitu kiwe kweli au si kweli, sharti iwe kauli. Kauli hii sharti iwe inarejelea kitu kilichopo katika ulimwengu ambamo kauli hiyo imetolewa. Maelezo ya Blocker (1970) hayatupi ungavu kuhusu dhana ya "kitu" aidha hatupati ufafanuzi wa kauli anazozirejelea. Makala hii inatumia kauli zinazorejelea usawiri wa maeneo na mianda ya kijamii inayovyazwa katika maeneo hayo ya kijiografia kwa mujibu wa nadharia ya uhakiki-maeneo.

Currie (1986) anaeleza kuwa, kuchanganua, kutathmini au kufurahia kazi simulizi bunilizi inatupasa kutenga kutoka matini ya hadithi, matukio pamoja na muktadha ambamo matukio haya yanatokea. Aidha, anaongeza kudai kuwa, ukweli katika bunilizi hausemwi wote katika bunilizi zenyewe bali baadhi ya mambo mengine huachiwa msomaji ajijazie. Makala hii inakubaliana na madai ya Currie (1986) kuwa kuna ukweli katika bunilizi. Hata hivyo, Makala inajikita katika usawiri wa mwandishi wa hadithi ya Mwendawazimu bila kujadili yale ambayo msomaji atajidadavulia kutokana na usomaji wake.

McFall (2003) anaeleza kuwa, baadhi ya bunilizi huwa zinajihusisha na ukweli ambao ni muhimu. Kwa hivyo, kuchunguza vile bunilizi zinavyovyaza ukweli, tunaweza kujifunza kitu na kutathmini ukweli mwenyewe. Makala hii itatumia uhakiki-maeneo kama kiunzi cha kuthaminia ukweli katika hadithi ya Mwendawazimu.

Gatzia & Sotnak (2014) wanaeleza kuwa, tunaposoma hadithi bunilizi tunatumia kichakatuzi cha kujibia swali kuwa, tunachosoma ni ubunifu au ni sehemu ya hadithi ambayo tunasoma. Wanaendelea kudai kuwa, kutathmini kauli zipi ambazo ni kweli katika hadithi tunahitaji kutumia masharti ya ukweli. Masharti ya ukweli wanayorejelea Gatzia na Sotnak yanajikita katika nadharia ya semantiki na Ulimwenguni Mwingine (Possible World Theory) ambayo ni tofauti na nadharia ya uhakiki-maeneo ambayo tutatumia kuchunguza ukweli katika uwasilishaji maeneo na mianda ya kijamii katika maeneo hayo ya kijiografia.

Wiese (2015) anaeleza kuwa kuna mantiki fulani kuhusu dhana ya ukweli ambayo inasaidia kugawa kazi za kibunilizi na kazi zisizo za kibunilizi. Mantiki haya yanatufanya kung'amua madai ya ukweli katika ugawaji huo. Anaendelea kudai kuwa, kazi mahuluti zinatumia ukweli kama kigezo cha kutenganisha ubunifu na ukweli katika mukutadha wa kazi zisizo kuwa za kibunilizi au kazi za kibunilizi, ili kutushajiisha kufikiria kuhusu kweli na ubunifu. Mantiki ambayo itajikita kwayo yanatokana zoezi la uhakiki-maeneo.

### 2.1. Nadharia ya Uhakiki Maeneo

Uchambuzi wa Makala unaongozwa na nadharia ya uhakiki-maeneo. Mwasisi wake ni Bertrand Westphal (2007) & (2011). Washirika wake Prieto (2011, 2016) na Tally (2011a, 2011b), walitafsiri kazi zake Westphal (2007) kutoka Kifaransa hadi Kiingereza.

Nadharia ya uhakiki-maeneo huchunguza maeneo ya kijiografia katika kazi za kibunilizi. Tally (2011a) na Prieto (2011), wameeleza kuwa, uhakiki-maeneo una mihimili mitatu. Mihimili hii ni dhana ya mwanda-wakati; ukiukaji mipaka na urejelezi. Dhana ya mwanda-wakati inahusishwa na ufululizwaji kati ya mwanda na wakati. Kuwa data za kimwanda zinasababisha uondoaji wa mipaka katika matini za kifasihi (Deterritorization). Huku dhana ya ukiukaji mipaka, mwanda huvuka mipaka ya kaida zilizokwishawekwa na kujenga mahusiano mapya kati ya watu, mahali (maeneo) na vitu (maumbile), (reterritorization). Nayo, dhana ya urejelezi ni uhusishwaji kati ya ulimwengu halisi kama tuujuavyo na matini. Mhakiki-maeneo huchunguza maeneo kama yalivyosawiriwa katika kazi za kifasihi.

Zao la uwasilishaji maeneo katika matini za kifasihi huvyaza aina tatu za uwasilishaji: kihomotopiki, kiheterotopiki na kitranto. Uwasilishaji wa kihomotopiki ni kuwasilisha mahali katika kazi za kifasihi kama tunvyopafahamu mahali katika ulimwengu halisi. Huku uwasilishaji wa kiheterotpiki ukihusisha uwasilishaji mahali tunapopafahamu kwa njia tofauti. Nao uwasilishaji wa kitranto, uwasilishaji wa kubunilizi kama katika kazi za kinjozi katika fasihi.

Wanauhakiki-maeneo hutumia mikakati ya mtizamo-kwingi, fahiwa ainati, mpangilio safu na mwingiliano wa matini. Mkakati wa mtizamo-kwingi huhusisha eneo kuchunguzwa kutoka mikabala mbalimbali. Fahiwa ainati inahusisha kuchunguza eneo kupitia fahiwa za uoni, unusi, hisi, mwonjo na usikivu. Mwingiliano matini huhusisha matini zinazoelezea eneo fulani kwa pamoja. Mpangilio-safu huchunguza historia ya maeneo yanayochunguzwa. Nadharia hii inasadifu kuchanganua ukweli-bunilizi katika hadithi ya "Mwendawazimu". Uchanganuzi huu utahusisha maeneo na mianda ya kijamii katika hadithi ya "Mwendawazimu".

## 3. Njia na Mbinu za Utafiti

Utafiti wa makala hii ni utafiti usiokuwa wa kitakwimu. Utafiti ulifanywa maktabani. Hadithi ya Mwendawazimu iliteuliwa kimakusudi na kusomwa pamoja na vitabu, majarida. Ihaji na wengine (2024) wakimrejelea Simiyu (2021) wanasema usampulishaji wa kimatilaba ni mbinu ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua kimaksudi sampuli anayotaka kwa ajili ya kukidhi malengo ya utafiti wake. Aidha, usakuraji wa tovuti ulifanywa ili kupata kufahamu mada vizuri.

Ulihusisha kusoma, kuhakiki na kutoa maelezo kuhusu swala la utafiti. Utafiti ulihusisha usampuli maksuudi. Kwa kuteua hadithi fupi ya "Mwendawazimu" ambayo ilikuwa na nduni nyingi za uhalisia katika maisha ya kimji. Kwa kutumia nadharia ya uhakiki-maeneo, data ilivyovyazika kupitia usomaji wa kina wa hadithi, ilifanyiwa uhakiki kubainisha swala la utafiti. Matokeo yake yaliwasilishwa kupitia maelezo. Kisha, mahitimisho kuhusu ufaafu wa nadharia ya uhakiki-maeneo katika kujenga kweli-bunulizi katika hadithi fupi ya "Mwendazimu" yalifikiwa. Makala hii, inanuia kuwapa changamoto watafiti wa fasihi ya Kiswahili, kudadisi kuhusu mada ya kweli bunilizi katika hadithi.

## 4. Uhakiki Maeneo Katika Hadithi ya Mwendawazimu

Katika sehemu hii tutachunguza nduni zifuatazo za uhakiki-maeneo: uwasilishaji, ukiukaji mipaka, mwingiliano matini, mpangilio-safu wa maeneo, fahiwa ainati katika hadithi, na mtazamo-kwingi wa mwandishi kama zinavyojitokeza katika hadithi ya "Mwendawazimu".

### 4.1. Uwasilishaji wa maeneo katika hadithi ya "Mwendawazimu"

Tally (2011a) ameeleza kuwa maeneo yanaweza kuwasilishwa katika matini za kifasihi kutumia mbinu za kitranto, homotopiki ama heterotopiki. Mbinu hizi za uwasilishaji zinapatikana katika hadithi ya "Mwendawazimu." Uwasilishaji wa hadithi ya "Mwendawazimu" umejikita katika maeneo mapana makuu: mjini Nairobi na Kangundo. Eneo la Nairobi mjini ndilo limeangaziwa sana huku eneo la Kangundo likirejelewa kwa uchache. Maeneo mahsusi katika Nairobi ambayo yameshughulikiwa ni pamaoja na eneo la buchari ya Matigari, barabara ya Moi, kituo cha magari cha *Tea Room na Kavuluka Ka City*, benki, kituo cha polisi cha Muthaiga na hospitali ya Mathare. Kadhalika, kuna eneo la ndani ya matatu ya *Kavuluka Ka City*. Katika maeneo haya, matukio mengine yanatokeo.

Katika maeneo haya ya Nairobi, kunayo yaliyowasilishwa kihomotopiki, kiheteropiki na kitranto. Maeneo yaliyowasilishwa kihomotopiki yaani jinsi yalivyo katika ulimwengu halisi ni pamoja na barabara ya Moi ambako mwanadada aliporwa elfu hamsini na majambazi akitoka benki (uk 2). Eneo jingine ni kituo cha magari cha *Tea Room*, ambapo bwana mmoja alilaghaiwa na "makasisi" kuwa wangemrudufishia pesa zake. Wizi huu unatokea katika kichochoro karibu na kituo hicho cha magari. Maeneo mengine ni kituo cha polisi cha Muthaiga na hospitali ya Mathare. Maeneo haya ndipo mzee Katona aliposhukishwa garini na wale waliojidai kuwa jamaa zake. Akiwemo mama mjamzito, wanaume wawili; mmoja akijidai kuwa kasisi. Nje ya hospitali ndipo alipopigwa goti la tumboni akaishiwa nguvu kisha akaibiwa pesa zake za kiinua mgongo. Wapita njia walifikiria ni kisa kingine cha mgonjwa kukataa kuingizwa hosipitalini.

Uwasilishaji wa kiheterotopiki unatokea katika maeneo kadha vile vile. Eneo la buchari ya Matigari ni eneo ambalo bila shaka wasomaji watalitambua japo si moja kwa moja. Maeneo kama haya ya ulaji wa nyama ya bei rahisi ni maarufu sehemu za mijini hasa Nairobi. Wasafiri na washitiri wengine hushabikia maskani haya. Eneo la benki pia limetokea hadithini kuwili. Licha ya kuwa, hatukupewa maelezo kuhusu benki ambayo mwanadada aliyeporwa elfu hamsini katika barabara ya Moi alikuwa ametoka. Aidha, hatujapewa maelezo ya

benki ambamo mzee Katona alipata laki za mbili za kiinua mgongo (*Golden Handshake*). Hatimaye kuna kituo cha matatu ambapo Kavuluka Ka City hubebea abiria wa kuelekea Kangundo. Tunaelezwa katika ukurasa. 2 (uk 2) kuwa, "*…alipenda [mzee Katona] kuisafiria katika safari zake za Kangundo na Nairobi*."

Matukio katika matatu ya *Kavuluka Ka City*, kutokea mzee Katona alipopanda matatu hiyo ikiwa imebakisha abiria wanne, hadi kufika kwa "jamaa" za mzee Katona; mama mjamzito na mshirika wake wa kiume. Hatimaye "Kasisi" kujiunga nao na kumshawishi kondakta, dereva na abiria kuwa mzee Katona ni mgonjwa apelekwe hosipitali ya Mathare, kisha kumhasiri mzee Katona na kumwibia nje ya hosipitali ya Mathare ni uwasilishaji wa kitranto. Hatuna uhakika wa kutukia kadhia hiyo. Huenda ukawa ubunifu wa mwandishi ili kufikisha ujumbe wake kwa wasomaji. Uwasilishaji huu unaenda kinyume na kanuni za ukweli katika bunilizi. Kwa hivyo, data yake haiwezi kutegemewa kuwa kweli.

Maeneo ya Kangundo na Tala yametajwa tu. Japo, ni maeneo ambayo ni halisi lakini hatuoni uwasilishaji wake ambao unaweza kutupa viashirii vya kuyachaganulia. Isipokuwa, nasaha za mkewe mzee Katona kuwa waandamane Nairobi ili kulinda pesa za kiinua mgongo. Jambo ambalo mzee Katona alilipinga. Katika (uk 3) anawaza kuwa, "Tangu lini mwanamke akawa mlinzi wa mwanamume kumkinga katika hatari?" Maelezo haya yanaashiria hofu ya watu wanaoishi viungani mwa mji wa Nairobi kuhusu swala la uhalifu wa mji huu.

5.2 Ukiukaji mipaka katika hadithi ya "Mwendawazimu"

Prieto (2011) anaeleza kuwa uhakiki-maeneo kupitia ukiukaji mipaka unaweza kutufunulia mambo ambayo hatukupata kuyajua katika maeneo ambayo tulifikiria mipaka yake ni madhubuti. Kumbe kuna vile mianda katika maeneo haya inaonyesha nduni ya uolevu. Dhana hii inaweza kuhusishwa kadhalika mianda katika maeneo ya hadithi ya "Mwendawazimu".

Katika eneo la buchari ya Matigari, tunalitarajia kuwa eneo la kuuza na ulaji nyama. Ulaji chamcha hapa ni jambo halali. Lakini mipaka ya uhalali inakiukwa wakati ambapo supu rojo inaugeuzwa na kuwekwa vidonge vya afyuni ili kuwalevya wateja. Katika (uk 1-2) tunaelezwa kuwa;

> …ni supu rojo tu kwa mgeni wa mahali hapa asiyefahamu magendo yanayoendelea kisiri. Kwa kuonyesha ishara fulani au kuagiza kwa lugha ya siri, mteja anaweza kuwekewa vidonge fulani vya afyuni kwenye supu yake akalewa kwa kuinywa. Dondoo 1(Kur.1-2)

Magendo haya ni kinyume cha matarajio ya jamii. Ufichuzi huu unatufanya kuelewa namna nyingine ya kuuza na kutumia dawa za kulevya kuliko tulivyodhani tunajua hapo awali.

Aidha, katika buchari ya Matigari kunatokea ufuska baina ya maborobaro wawili na Bi. Pandikizi. Licha ya kuwa mkahawa uliojaa pomoni, katika (uk 2) tunaelezwa kuwa, barobaro mmoja alikuwa amepenyeza vyanda vyake kwenye kifua cha Bi. Pandikizi ambaye kizibao alichokuwa amevaa hakikusitiri mwili wake vyema. Hatimaye baada ya kubugia supu rojo yenye afyuni, tunaelezwa katika (uk 5) kuwa, "Bi. Pandikizi sasa kalewa chopi…mara waliamuka [mabarobaro] na kuanza kuondoka wakiwa wanamhangahanga mwanamama huyo…kondoo kajitia mwenyewe mikononi mwa chui kukumbatiwa". Kumbe chamcha na maskani yake yamegeuzwa mahali pa kufanya vitendo vya kuhuni.

Kadhalika, asasi ya dini imekiuka mipaka yake. Makasisi bandia ndio wanaoibia watu pesa zao. Raia wanawamini kumbe ni wezi. Katika eneo la kituo cha magari cha Tea Room, "Makasisi" walimghilibu bwana mmoja kuwa wangemrudufishia pesa zake. Walitoweka na pesa hizi walipokuwa wakisali. Bwana huyo alipofungua macho na kusema Amen, hakupata pesa zake, viatu wala "Makasisi". Hata mzee Katona aliibiwa kwa msaada wa "Kasisi" aliyejidai ni jamaa yake. Aliwarai abiria wasaidie kumshukisha mzee Katona walipofika karibu na hospitali ya wagonjwa wa akili ya Mathare. Huyo "Kasisi" ndiye alimpiga mzee Katona goti la tumboni ili wamwibie. Vitendo vya kuwaibia watu vinakiuka hadhi na mbeko za kisasi tujuavyo. Vitendo hivi vya "makasisi" mbinu mpya ya wizi katika mianda tuliojadili. Hivyo, kujenga kiunzi cha ukiukaji-mipaka.

Dhana ya Matigari inahusishwa na mwandishi Ngugi wa Thiong'o (1986). Katika riwaya yake yenye jina hilo, alimsawiri mhusika jagina ambaye alikuwa na mizungu mingi. Vivyo hivyo, hadithi ya "Mwendawazimu" imesawiri buchari ya Matigari ambayo inasifika kwa nyama freshi na bei ya chini. Katika vyumba vya buchari yenyewe kuna mizungu kupitia matendo ya wahusika mbalimbali. Hivyo, kuna ukuruba mkubwa kihulka katika Matigari mhusika na Matigari eneo. Kwa mujibu wa wanamwingiliano wa matini, ni fenomena ya urejelezi wa matini, kunukuu au kugusia matini nyingine. Mwingiliano matini ni uhusiano wa matini katika viwango tofauti, ambapo uelewa wa matini moja unashawishiwa na matini nyingine (Allen 2000)

### 4.2. Mpangilio-safu wa maeneo katika hadithi ya "Mwendawazimu"

Dhana ya mpangilio-safu kwa mujibu wa Prieto (2011) inahusu vipindi mbalimbali vya historia ya maeneo tunayochunguza hadithini. Kupitia mzee Katona tunapata uwasilishaji wa mji wa Nairobi katika vipindi tofauti. Kwanza, yamkini kulikuwa na visa vya wizi zama za mzee Katoni akifanya kazi Nairobi. Katika (uk 3) tunaelezwa kuwa, "*Katika miaka yote alivyokuwa akifanya kazi mjini Nairobi, hakuwahi hata siku moja kuhadaika kwa mbinu za majambazi*". Mkewe mzee Katona Ndunge alipomrai wandamane Nairobi, mzee Katona alikataa ombi hilo. Kwa kuwa alijiamini sana, katika (uk 4) tunaelezwa kuwa, "*Aliamini kwamba angeweza kutambua jambazi yeyote aliyetaka kumvizia*". Kumbe mbinu za mzee Katona za kutambua ujambazi zilipitwa na wakati. Wezi walikuwa wameimarika na kuzua mbinu mpya za kuiba. Si ajabu kwamba, mzee Katona hakung'amua 'sadfa' ya kufuatana na mama mja mzito na mshirika wake wa

kiume kutoka benkini hata Matigari na matatu aliyoabiria kurejea kwake. Kutokana na maarifa ya wezi hao walifaulu kuwaghilibu kondakta, dereva na abiria wa matatu kuwa mzee Katona alikuwa muwele wa akili, hadi wakapelekwa karibu na hosipitali ya Mathare ambapo walimshukisha mzee Katona kwa msaada wa abiria wenzake na kumwibia. Jitahidi za mzee Katona kukanusha kuwa hakuwa babake mzazi wa mwizi alijidai kuwa mja mzito hazikufua dafu.

Matukio katika wizi wa fedha za mzee Katona ni ishara tosha kuwa mji umebadilika. Hata wezi wamekuwa wabunifu zaidi. Wanakuibia mchana peupe pasi na wasiwasi wowote kadmnasi ya watu.

Mabadiliko mengine ni kutokana na tehama wakati huu dhidi ya miaka ya mwanzo 1990 ambako ustaafishaji wa wafanyi kazi mapema al maarufu kama *Golden Handshake* ulishamiri. Kukosekana kwa Tehama iliyoimarika, ilibidi mzee Katona kutoka Kangundo hadi Nairobi ili apate kiinua mgongo chake. Katika enzi hizi za Tehama, mtu anaweza kupokea fedha zake hata katika rununu yake. Kipindi hicho cha usungo wa kidijitali kinarahisisha wazee kama Katona kuibiwa pesa zao mjini kutokana na ujanja wa majambazi ambao wanawavizia.

### 4.3. Fahiwa ainati katika hadithi ya "Mwendawazimu"

Prieto (2011) anabainisha kuwa, ili kufikia lengo lake, uhakiki-maeneo unahusisha matumizi ya fahiwa za kuona, kusikia, kuonja, kuhisi na mwendo. Hadithi ya "Mwendawazimu" inaafiki kipengee hiki cha fahiwa ainati.

Hadithi ya "Mwendawazimu" imesheheni viashirii vya fahiwa ainati ambavyo vinasaidia kufasiri hadithi yenyewe. Kwanza, kuna matumizi ya fahiwa ya kuona. Katika buchari ya Matigari tunauona umayamaya wa washitiri. Wengine hata hawana mahali pa kukaa. Baroboro mmoja alikuwa ameweka mkono wake katika kifua cha Bi. Pandikizi.

Pili, kuna fahiwa ya mwonjo. Chakula cha Matigari kinaelezwa katika (uk 2) kuwa, ni "*freshi siku zote*". Aidha, kuna supu rojo (uk 1). Mzee Katona katika (uk 6) tunaelezwa kuwa, "*Alidondoa kipande cha nyama na kuitia mdomoni. Nyama yenyewe ni laini kweli…Astaa…si utamu huo!*"

Nayo fahiwa ya hisi inapatikana kupitia pigo la mzee Katona. Katika (uk 10) tunaelezwa kuwa, "Kasisi alimshika mzee Katona shingoni na kumrushia goti kali kwenye tumbo." Bila shaka mzee Katona aliona uchungu mwingi. Machungu haya yaliwarahisishia wezi kumpokonya mzee Katona kibunda chake cha pesa.

### 4.4. Mtazamo-kwingi katika hadithi ya "Mwendawazimu"

Prieto (2011) anaeleza kuwa, mbinu mojawapo wanayotumia wanauhakiki-maeneo kufikia malengo yao ni Mtazamo-kwingi. Kwamba, waandishi tofauti wanaweza kutupa mwanga kuhusu eneo moja. Anatoa mfano wa mji wa Paris, namna ulivyosawiriwa na waandishi tofauti unatupa data nzuri ya kuujenga tena mji huo, hata kama ungetoweka ulimwenguni. Hata hivyo, makala hii ina maoni kuwa, eneo fulani linaweza kuvyaza mianda tofautitofauti hivyo kuafiki maelezo ya mtazamo-kwingi. Mathalan, vitendo vya wizi katika eneo la mji wa Nairobi limeangaziwa na mwandishi kupitia mikabala tofauti. Upo wizi wa kuviziwa na majambazi na kuporwa ulichobeba. Mfano mzuri ni ule wa mwanadada aliyeporwa katika barabara ya Moi. Kadhalika, upo wizi wa kughilibiwa kisa wezi wanatoroka na pesa zako. Bwana aliyeghilibiwa katika vichochoro vya eneo la *Tea Room* na "makasisi" wa sala ni mfano mzuri. Halafu, upo wizi wa mabavu, kama aliyotagusana nao mzee Katona.

Pili, mwandishi amesawiri maisha ya maeneo ya mashambani na mjini. Mashambani kama Kangundo kunaonekana kutulivu. Mzee Katona alipostaafu alielekea huko. Hata alikuwa na ndoto ya kufungua biashara yake katika eneo la Tala. Ili kutimiza ndoto ya ujana wake ya kujifungulia biashara (uk 5 -6). Kwa hivyo, eneo la mashambani yamkini ni la kutimiza ndoto za mtu. Mjini Nairobi kuna makuruhu na visa vingi vya ujambazi. Visa hivi vinaonekana kukwamiza ndoto za watu. Mzee Katona na ndoto yake ya kufungua biashara iliisha kwa kupokonywa kiinua mgongo chake.

## 5. Hitimisho

Kutokana na mjadala huu kuhusu nduni za uhakiki-maeneo katika hadithi ya "Mwendawazimu" na jinsi ukweli unavyodhirika kutokana na uwasilishaji maeneo na mianda katika maeneo hayo, ni dhahiri kuwa maeneo yakini yamewasilishwa hadithini kiyakinifu. Maeneo hayo ni kama vile Kangundo, Tala, barabara ya Moi, kituo cha polisi cha Muthaiga na hosipitali ya Mathare. Mbali na maeneo kuna matukio katika maeneo mbalimbali ambayo ni halisi. Mathalani, matumizi ya dawa za kulevya, wizi ainati, ufuska, taasubi ya kiume na udanyanyifu yametokea hadithini.

Ufanifu wa uhakiki-maeneo umetusaidia kufasiri hadithi hii kwa undani. Kutokana na ukweli katika kazi hii ya kibunilizi. Hivyo, kuthibitisha Tasnifu yetu kuwa, uhakiki-maeneo ni zoezi ambalo linatekeleza wajibu mkubwa katika kutathminia ukweli katika kazi za kibunilizi kama hadithi fupi za Kiswahili. Kama tulivyofanya kupitia kielelezo cha hadithi fupi ya "Mwendawazimu".

Utafiti huu, unapendekeza yafuatayo: Vipengee vingine vya kibunilizi kama wahusika vichanganuliwe kwa kutumia kanuni za uhakiki-maeneo. Uhakiki-maeneo liwe zoezi la kuchanganulia hadithi fupi za Kiswahili. Eneo moja mahsusi kama mji wa Nairobi katika bunilizi lihakikiwe kiuhakiki-maeneo. Kipengele cha uhakiki-maeneo cha mpangilio-safu kichunguzwe zaidi kinaweza kuvyaza data za kihistoria katika maeneo ambayo tulidhania tunayafahamu vyema.

## Marejeleo

Allen, G. (2000). **Intertextuality**. Routledge: New York.

Blocker, H.G., (1970). The Truth about Fictional Entities. The Philosophical Quarterly (1950), 24 (94), 27 – 36. https;//doi.org/10.2807/2218282

Currie, G. (1986). Fictional Truth Philosophical Studies: An International Journal for Philosophy in Analytic Tradition, 58(2) 195 -212. https://www.jstor.org/Stable/4319855

Gatzia, D. E. & Sotnak, E. (2014). Fictional Truth and Make-Believe. Philosophia 42, 349 – 361. https://doi.org/10.1007/s//406-013-9511-9

Ihaji,K; Miruka,F.& M'Raiji, J.(2024). Matumizi ya Mkabala Njia Mseto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Upili. Jarida la Kiswahili Sanifu Toleo 1: 1-7

Mbatiah, A. M. (1996). "Jahanamu". Katika K. King'ei na R. M Wafula, Pendo la Heba na Hadithi Nyingine, (uk 44 - 50). University of Nairobi Press: Nairobi.

Mbuthia, E.M. (2005). A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories. VDM Verlag Muller GmbH & Co: Deutschland Germany.

McFall, L., (2003). Fictional Truth. In Educational Knowledge and Truth (pp 110 – 127). Routledge: New York.

Ngugi wa Thiong'o (1986). Matigari. Penguin Random House: New York.

Prieto, E.(2011). Geocriticism, geopolitics, geophilosophy and beyond. Katika *Geocritical explorations: Space,Place and mapping in Literary Studies* (uk 13-27). New York: Palgrave Macmillan US.

Prieto, E. (2016).Geocriticism meets Ecocriticism: Bertrand Westphal and Environmental Thinking. Katika Tally,R.T., Battista, C.M. (Wh) Ecocriticism and Geoctiticism. Geocriticism and Spatial LiteraryStudies. Palgrave Macmillan, New York. https://doi.org/10.1057/97811375542625-2

Roberts, V.E & Jacobs, H.E (1995). Literature: An Introduction to Reading and Writing.Prentice Hall: New Jersey

Shake, R. (2000). "Mwendawazimu" katika Mbatiah M. (Mh). Mwendawazimu na Hadithi Nyingine. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Sharobeem, H. (2015). Space as the Representation of Cultural Conflict and Gender Relations katika Kutoka: http://www.jastor.org/stable/24372861

Simiyu,B.W.(2022).Gaps in Informed Consent Process among Women who have undergone Elective Caeserean Section at AIC Kijabe Hospital, Kiambu County (Doctoral Dissertation)

Tally, R., (Mh.). (2011a).Introduction. Katika Geocritical Explorations: Space, Place and Mapping in Literary and Cultural studies: Palgrave Macmillan: New York https://doi.org/10.1057/97802303337930 1

Tally,R.(2011b). On Literary Cartography:Narrative as a Spatially Symbolic Act. Katika,New American Online https://nanocriit.com

Wiese, A. (2015). Telling what is true: Truthfulness and Fictional Truth in Hybrid (non. Prose Structure, 3791), 66 -82. https://doi.org/10.1080/01440357.2015.1056489

Westphal, B. (2007). Géocritique; réel, fiction, espace. Paris: Minuit.

kWestphal, B. (2011). Geocriticism: Real and Fictional Spaces. Wah. Robert T. Tally. New York: Palgrave Macmillan.